

SHEIKH SA'D AL-HUSAYN

(hafidhahullâh)

KUMUHUSU SHEIKH 'ALI HASAN AL-HALABI AL-ATHARI NA MASHEKHE WA KI-SALAFI WA JORDAN

Mfasiri: Abu Farida Muhammad Awadh Salim Basawad

Taarifa hii inaweza kupatikana hapa:

<http://file14.9q9q.net/Download/74933655/11.ram.html>

Sheikh Sa'ad bin 'Abdur-Rahmân al-Husayn (*hafidhahullâh*), akiwa kwenye mazungumzo kwa njia ya simu alikusudia kupata ukosoaji wa Sheikh 'Ali Hasan, alimsifu Sheikh 'Ali na akamkosoa muulizaji! Amesema Sheikh Sa'ad al-Husayn:

- ❖ "Ni nani huyo aliyesema yakuwa ati wao kazi yao ni kujificha nafsi zao tu ndani ya U-Salafiyah? 'Ali Halabi na ndugu zetu ni miongoni mwa *ma-du'ât* walio bora katika Sunnah kutokana na tunayoyajua sisi na malipo yao yako kwa Allâh."
- ❖ "... na dalili ni kwamba mimi nimekuwa pamoja na wao kwa nusu Qarne na robo ya Qarne, na nimekuwa nikiwafuatilia na nimeona waliyozalisha na mimi nashirikiyana nao."
- ❖ "Mimi sijaona yakwamba ati wamebadilika mpaka leo hii..."
- ❖ Kisha, al-'Ârif akamwambia Sheikh Sa'ad: "Wewe ulikuwa ni mwangalizi wa Sheikh Bin Bâz!" Sheikh Sa'ad akajibu suala hilo kwa kusema: "Mimi sijawahi kuwa ni mshauri wa Sheikh Ibn Bâz wala mtu mwengine yoyote..."
- ❖ Kulingana na rai yangu (hawa Mashekhe wa Jordan) walioko Shâm ndio walio bora zaidi katika Manhaj na shughuli za ki-Da'wah."
- ❖ Vilevile Sheikh Sa'ad akamwambia al-'Ârif: "Kwa bahati mbaya, wewe inaonekana kana kwamba unawachagua Ahlus Sunnah walioko Misri, Jordan na hata Palestina na kwa ajili ya muelekeo huu unawaondoa (*ma-Salafi*) wengi wao waliokuzingira wewe."

- ❖ Mimi simjui 'Ali al-Halabi kuwepo kwenye mkondo wa Manhaj ya Sayyid Outb, bali amemrudi yeye kwa mara nyingi kuliko ulivyofanya wewe (al-'Ârif)!"
- ❖ Kisha hatimae, Sheikh Sa'ad akamwambia al-'Ârif: "...kwahivyo wewe wanizuiya mimi kutofanya shughuli zangu nilizokuwa nikifanya." na kumaliza mazungumzo hayo!

Sheikh Sa'ad alihitimu kutoka katika Chuo Cha Shari'ah, Makkah mnamo 1376 AH, kisha akasoma fasihi ya Kiarabu katika Chuo Cha Masomo ya Juu ya Kiarabu mjini Cairo, na vilevile akasoma katika Chuo Kikuu Cha Southern California. Yeye alikuwa ni msimamizi wa da'wah katika Balozi za Saudi Arabia zilizoko Shâm kuanzia mwaka wa 1401-1422 AH. Yeye ametunga, akakusanya na kuandika idadi ya vitabu kikiwemo kitabu maarufu cha kumkosoa Sayyid Outb kitiwacho *Fikr Sayyid Outb Bayna Ra'ayn* [Fikra za Sayyid Outb baina ya rai mbili]. Orodha kamili ya vitabu vyake yaweza kuonakana hapa: <http://www.saad-alhusayen.com/content/6>

Katika majadiliano ya simu ya hapo juu, muulizaji si mwengine bali ni Mhasibu kutoka Palestina, aitwae Hishâm bin Famhi al-'Ârif, ambaye kujulikana kwake kumetokana na Mashayekh wa Jordan tu, na alikuwa ni mwanafunzi wao! Vilevile inashangaza kuona yakwamba ametayarishwa na kufanywa kuwa ni Sheikh naye, haliyakuwa katika wakati alipokuwa akisafiri kwenda Luton nchini Uingereza, na QSS nchini Canada, sauti hizohizo ambazo zinazomshangilia maneno yake hazikuwa zikikubali chochote kutoka kwake hapo!

Sheikh Sa'ad alikuwa kwenye balozi za Shâm wakati huo.

Jambo la kushangaza ambalo al-'Ârif alikuwa akijaribu kulifanya ni kuonyesha kwamba Sheikh 'Ali Hasan yuko juu ya Manhaj ya Sayyid Outb!!??